2017

# MKATABA WA UBIA WA UCHIMBAJI MADINI

KATI NA BAINA YA

RUBY INTERNATIONAL LTD

NA

PASKARI JONAS MPANDULE, MATHEW ALEX NGONYANI
BENJAMIN MAKOTI NA YASIN MUSSA SALAMU

# MKATABA WA UBIA WA UCHIMBAJI MADINI

KATI NA BAINA YA

RUBY INTERNATIONAL LTD

NA

PASKARI JONAS MPANDULE, MATHEW ALEX NGONYANI,
BENJAMIN MAKOTI NA YASIN MUSSA SALAMU

JANUARI, 2017

# MKATABA WA UBIA WA UCHIMBAJI MADINI

**MKATABA** huu wa Ubia wa Uchimbaji madini umefanyika leo tarehe 10 mwezi Januari mwaka 2017.

**KATI NA BAINA YA**

***Mathew Alex Ngonyani, Benjamin Makoti, Yasini Mussa Salum na Emmanuel Jonas Mpandule wa S.L.P 8, Mahenge/Ulanga, Morogoro,Tanzania (ambao*** ndani ya mkataba huu watajulikana kama ***"Wenye Leseni"*** tamshi ambalo pale inapobidi itajumuisha ***warithi*** wao) ambao wanawakilishwa na ***Mathew A. Ngonyani*** kwa upande mmoja.

**NA**

***M/S RUBY INTENATIONAL LTD, wa S.L.P 149, Mahenge/Ulanga, Morogoro, Tanzania*** (ndani ya mkataba huu itaitwa ***"Mwekezaji"***, tamshi ambalo pale inapobidi itajumuisha ***mrithi*** wake) ambayo inawakilishwa na ***Salim A. Hasham na Betold T. Matamba*** kwa upande mmoja.

KWA KUWA:

A. kikao cha makubaliano ya Uchimbaji wa Madini ya Vito na kukubaliwa na pande zote mbili ***"Wawekezaji"*** na ***"Mwenye Leseni"***.

B. **Mwenye Leseni** anajishughulisha na shughuli za uchimbaji madini.

C. **Mwenye Leseni** ni mmiliki halali wa ***Leseni ya Uchimbaji Madini Namba. PML 0007018CZ*, Epanko, Wilaya ya Ulanga, Mkoani Morogoro**, iliyotolewa na Wizara ya Nishati na Madini ya tarehe **27, Desemba 2016.** kwamba Mwenye Leseni na Mwekezaji wamelidhia kuendesha shughuli uchimbaji ya madini kwa ubia.

D. **Mwenye Leseni** anathibitisha kwamba mipaka yote imeonyeshwa kwa uwazi na kwa uhalali katika Leseni ya Uchimbaji Madini ambayo inatoa haki kwa aliye na leseni ya kuendesha shughuli za uchimbaji madini pamoja na shughuli nyingine zinazoendana nazo au zilizomuhimu kwa ajili ya uchimbaji madini; na

E. Uendelezaji wa mgodi wa madini ya vito una changamoto nyingi, unahitaji mapitio ya mara kwa mara juu ya malengo, mbinu au mipango katika shughuli za uchimbaji madini kwa kuzingatia mazingira hayo pande zote mbili ndani ya mkataba huu zimeamua kuingia katika ubia huu ili kujihakikishia uchimbaji wenye tija na wa haraka kwa maendeleo ya mradi; na

F. Kwa masharti yaliyomo ndani ya mkataba huu wahusika wamehiari kuingia mkataba wa ubia wa ***uchimbaji,na uuzaji wa madini kwa kadiri yatakavyo patikana.***

G. **Mwekezaji** yuko tayari kutoa fedha za mtaji wa kazi kwa ajili ya uchimbaji katika eneo la leseni kwa faida ya pande zote mbili ndani ya mkataba huu; na;

**KWA KUWA** pande mbili ndani ya mkataba huu wana nguvu za kitaasisi ambazo zikiunganishwa pamoja zitawezesha ufikiwaji wa madhumuni ya hapo juu, hivyo basi inakubalika kama ifuatavyo:-

1. **Kwamba Pande mbili** za mkataba huu wanakubaliana kwamba kwa pamoja watafanya utafiti na uchimbaji madini katika eneo la mkataba kama lilivyokubalika ndani ya mkataba huu.

2. **Kwamba pande mbili** za mkataba huu wataingia katika ubia mahsusi kwa ajili ya uchimbaji madini.

   (i) Inakubalika kwamba pande mbili za mkataba huu Mwekezaji ataleta mtaji, ubora, udhibiti wa viwango na teknolojia muhimu kwa mafanikio ya undeshaji wa mradi.

   (ii) Mwekezaji ataleta katika mradi timu ya ujenzi na ufundi yenye uwezo.

3. Mwenye Leseni atakuwa na jukumu kutunza nipaka ya leseni iwe katika hali nzuri kisheria kwa kulipa ada na kodi zote stahiki na kutimiza sheria na kanuni zinazo simamia masharti ya kutolewa kwa leseni.

4. Inakubaliwa kuwa asilimia 40% ya gawio litachukuliwa na Mwenye leseni na asilimia 60% ya gawio litachukuwa na Mwekezaji bila kuondoa gharama za uendeshaji.

Kwa kuondoa utata mgawanyo utakuwa kama ifuatavyo:-

(i) Mwenye Leseni gawio la asilimia 40%
(ii) Mwekezaji gawio la asilimia 60%

5. Kwamba madini yatakapopatikana **Mwekezaji** atakuwa na haki ya kwanza ya kuyanunua.

6. Mkataba huu wa ubia wa uchimbaji madini umefungwa kwa maelewano kuwa Mwenye Leseni anachangia eneo lake la uchimbaji madini na kwamba Mwenye Leseni hatachangia fedha, na kwamba vyanzo vyote vya fedha katika mradi huu zitatolewa au kugharamiwa na Mwekezaji.

7. Kwamba kila upande utahakikisha utatunza taarifa au siri zote za uendeshaji wa mkataba huu bila kutoa kwa mtu yeyote asiyehusika isipokuwa tu kwa ridhaa ya kimaandishi kutoka kwa pande zote za mkataba au pale endapo ni lazima kufanya hivyo ili kutekeleza matakwa ya mkataba huu.

8. Mabadiliko ya masharti mkataba huu wa ubia ikiwa ni pamoja na marekebisho ya ukomo na wajibu wa wahusika wa mkataba huu yatatekelezwa tu pale pande zote za mkataba zitasaini.

9. Inakubalika kwamba pande zote za mkataba huu zitaunda Menejimenti Bodi ambayo itakuwa na nguvu, haki na uwezo wote wa kuongoza, kuamua na kuendesha mambo yote yahusuyo mradi huu wa uchimbaji madini. Pande za mkataba huu zinakubali kuwa ***Bw. Salim A. Hasham*** ataongoza na kuendesha shughuli za mradi huu kwa upeo wake wote kwa maslahi ya mkataba huu wa ubia.

10. **UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA UBIA**

Kwamba ubia huu utakuwa kwa kadiri ya makubaliano ya pande zote:-

(i) Meneja atawajibika kuhakikisha kila anapohitajika na wahusika kusimamia na kutoa taarifa kwa faida ya wabia wa mkataba huu.

(ii) Meneja atateuliwa na atawajibika kwa mjibu wa sheria ya madini (Mining Act) na kanuni zinazo simami shughuri za madini na atatunza kumbukumbu zote za malipo, risiti, vocha na nyaraka nyingine za fedha zinazohusiana na mradi huu wa ubia mpaka pale tu atakapoelekezwa tofauti na pande zote za mkataba huu.

11. Kwamba kila upande wanathibitisha kwamba una nguvu na uwezo wa kuingia katika mkataba huu na kutekeleza masharti na makubaliano ya mkataba huu.

12. Kwamba kila upande katika kipindi chote cha mkataba huu na hata pale utakapo koma utatunza mambo yote yatakayokuwa ni siri za ubia.

13. Hakuna upande wowote utakao ruhusiwa kutoa hadharani habari yoyote ya mkataba huu bila ya kupata ruhusa ya kimaandishi kutoka kwa wahusika wote.

14. Kwamba shughuli za mkataba huu zitaanza baada ya siku 90 toka tarehe ya kusaini mkataba huu ili kutoa nafasi kwa mwekezaji kwa ajili ya kutafuta na kujiweka tayari kuanza shuguri za uchimbaji.

15. Kwamba mara baada ya mkataba huu kuisha/kufikia mwisho kwa namna yoyote ile, chochote chenye kuhamishika kitakachokuwepo kwenye eneo la mgodi kitabakia kuwa mali ya mwekezaji na iwapo upande wa mwenye leseni utavunjika mkataba huu kwa namna yoyote ile kabla ya mkataba kufika mwisho wake kwa mujibu wa mkataba huu ama kwa namna nyingine yoyote ambayo haikusababishwa na mwenye leseni, basi mwenye leseni hatawajibika kulipa gharama zozote za uwekezaji zitaazokuwa zimefanywa na mwekezaji kwenye mgodi.

16. Kwamba mwekezaji atatakiwa kuanza shughuli za uwekezaji katika siku sitini (90) tangu tarehe ya kusaini mkataba huu baada ya kuwepo mazingira yanayoruhusu uwekezaji baada ya kuondolewa watu wengine wanaoendesha shughuli yoyote ile kwenye eneo la uwekezaji na hataruhusiwa kusimamisha uzalishaji/uwekezaji kwa zaidi ya siku sitini bila ya kuwepo sababu za msingi na iwapo itatokea hivyo basi mwenye leseni atatoa notisi ya siku sitini yenye kutaka kupewa sababu za kusimama huko na iwapo sababu zitakazotolewa siyo za msingi basi mwenye leseni atakuwa na haki ya kutoa notisi ya kusimamishwa mkataba.

17. Kwamba marekebisho au nyongeza yoyote ya mkataba huu yatafanya kazi ikiwa tu yatakuwa yamekubaliwa na kusainiwa na pande zote mbili.

18. **MASHARTI KWA WABIA**

Kila mbia anajifunga kwa mwenzake kama ifuatavyo:-

(i) Kutekeleza kila jukumu katika eneo la mradi kwa mujibu wa Sheria ya madini na sheria zinginezo.

(ii) Kutekeleza jukumu lake kwa ajili ya kutimiza mkataba unaohusisha ubia au shughuli za wabia.

(iii) Kutokufanya au kusababisha kufanyika jambo lolote ambalo litaathiri ubia huu au shughuli zake.

(iv) Kushirikiana kwa uaminifu kwa kila jambo linalohusu mradi wa ubia huu.

19. **MASHARTI YA MUDA WA MKATABA, KUSITISHWA, KUVUNJIKA KWAKE.**

(i) Mkataba huu utadumu katika kipindi chote cha uhai wa leseni cha miaka saba au vinginevyo uwe umeongezewa muda au umesitishwa kabla ya muda huo. Mkataba huu waweza kuendelezwa (renewed) baada ya kwisha kwa makubaliano mapya au kuendelea kwa masharti yaliyo ndani ya mkataba huu kama itakavyoonekana yafaa.

(ii) Kila upande wakati wowote wanaweza kukubaliana kwa sehemu mashariti ya ubia ya shughuli zote za ubia huu zisimame/zisitishwe kwa kipindi fulani kwa makubaliano ya pande zote mbili.

(iii) Mwekezaji atashindwa kuanza kazi za uchimbaji katika kipindi cha siku tisini (90) tokea kutiwa sahihi ya mkataba.

(iv) Kuwa mwenye mgodi atatoa notice ya siku sitini baada ya kuwekezaji atashindwa kuanza kazi katika kipindi cha siku tisini (60).

(v) Upande mmoja ukibainika na kuthibitika kuwa umejihusisha na wizi, na upande utakaodhihirika na kujihusisha na wizi wa madini yaliyopatikana utawajibika kurudisha pamoja na fidia.

(vi) Kwamba pale ambapo shughuli zote za uchimbaji madini yata kuwa ya mekwisha kwa mujibu wa ubia huu mkataba huu unaweza kutafsiriwa kuwa umekwisha kwa upande zote.

20. **MATATIZO YASIYO ZUILIKA AU YALIYO NJE YA UWEZO WA PANDE ZOTE ZA MKATABA HUU**

Wabia katika mkataba huu hawatawajibika kwa kushindwa kutimiza masharti au majukumu ya mkataba huu endapo:-

a) Kwamba kushindwa huko kumetokana na matatizo yaliyo nje ya uwezo wa mhusika.

b) Kwamba tatizo hilo halikutegemewa kutokea kwa namna yoyote wakati wa kusaini mkataba huu na kwamba hata athari yake haikueleweka kuwa inaweza kuathiri utendaji wa mbia.

c) Kwamba tatizo lililoko katika ibara ya 21 (a) linaweza kuwa limetokana na sababu kama vile vita, fujo, mapinduzi, migomo, matetemeko, mafuriko, radi, milipuko, moto na sababu zingine.

21. Kwamba **Mwenye leseni** hataruhusiwa kuhamisha kwa namna yoyote ile au kuuza, umiliki wa leseni au asilimia yoyote ya umiliki wake wakati mkataba huu ukiwa hai na pale inapotokea kwamba kuna umuhimu/ulazima wa mwenye leseni kufanya uhamisho wa hisa zote au sehemu yake, basi mwekezaji atakuwa na haki ya kwanza ya kununua/kupewa hisa zinazotarajiwa kuhamishwa/kuuzwa na iwapo haitawezekana mwekezaji kupewa/kununua na ikaonekana kwamba ni lazima hisa hizo zihamishwe au kuuzwa basi itafanyika hivyo baada ya kupata ridhaa ya maandishi ya Mwekezaji.

22. Kwamba kila upande utazingatia na kutimiza masharti maalum ya kutolewa kwa leseni ya uchimbaji wa madini pamoja na sheria mtambuka aidha za Serikali au Serikali za mitaa/ Halmashauri au mamlaka nyingine inayojihusisha na shuguri za utafutaji na chimbaji wa madini au sheria na kanuni taratibu zinazo ambatana na shughuli za utafutaji na uchimbaji wa madini, kulipa mrahaba/kodi, tozo/ada, kutekeleza makubaliano baina ya wabia au wawakilishi wake na kwamba tatizo lolote likitokea litapaswa kupelekwa kwa msuluhishi kwa mujibu wa sheria ya Usuluhishi (Arbitration) inayotumika Tanzania.

23. Mkataba huu utasajiliwa/kutambuliwa kwa mjibu wa sheria ya madini/msajiri wa hati.

**KUKAMILISHA MKATABA.**

Mkataba huu utasainiwa katika nakala nne zote zikiwa ni nakala halisi, na hauta tambua na utakuwa na nguvu dhidi ya mikataba/kufuta mikataba yote inayohusisha ama mikataba ambayo imewahi kuingiwa /kufanywa na wabia wa leseni tajwa hapa ndani ya mkataba huu kwa namna yoyote ile.

**KWA USHUHUDA**

***MKATABA umefanyika leo tarehe 10, Januari 2017, hapa Dar es Salaam.***

Mkataba huu umewekwa sahihi na
***MATHEW A. NGONYANI*** *ambaye*
*Ametambulishwa kwangu na* ***EMANUEL MAGAI***
Ambaye ninamfahamu leo tarehe 10 Januari, 2017.

**MATHEW A. NGONYANI**

**MBELE YANGU**

Jina kamili : INNOCENT P. MWELELWA
Sahihi :
Anwani : 12076 DSM
Wadhifa : MWAKILI

INNOCENT PAULOS MWELELWA ADVOCATE NOTARY PUBLIC & COMMISSIONER FOR OATHS P.O. BOX 12076, DAR ES SALAAM

Mkataba huu umewekwa sahihi na
**M/S RUBY INTERNATIONAL LTD**
ambaye ninamfahamu/ametambulishwa
**EMANUEL MAGAI** leo tarehe **10 Januari, 2017**.

Jina : **SALIM A. HASHAM**
Sahihi :
Anwani : P.O. Box 149 – Mahenge/ Morogoro
Wadhifa : Mkurugenzi

Jina : **BETOLD T. MATAMBALA**
Sahihi :
Anwani : P.O. Box 149 – Mahenge/ Morogoro
Wadhifa : Mkurugenzi

**MBELE YANGU**

Jina kamili : INNOCENT P. MWELELWA
Sahihi :
Anwani : 12076 DSM
Wadhifa : MWAKILI
Tarehe : 10/1/2017

INNOCENT PAULOS MWELELWA ADVOCATE NOTARY PUBLIC & COMMISSIONER FOR OATHS P.O. BOX 12076, DAR ES SALAAM